

BWANA AMEJAA HURUMA

D. Denis

S
A
B
T

Bwa na a me ja a hu ru ma na ne e ma, Bwa na a me ja a hu ru

ma na ne e ma.

NB: MASHAIRI YASOMWE KAWAIDA

1. Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana.
Naam, vyote vilivyo ndani yangu
vilihimidi jina lake Takatifu.
Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana,
Wala usizisahau fadhili zake zote.(Kiitikio)

2. Akusamehe maovu yako yote,
Akuponya magonjwa yako yote,
Aukomboa uhai wako na kaburi,
Akutia taji ya fadhili na rehema.(Kiitikio)

3. Bwana amejaa huruma na neema,
Haoni hasira upesi, ni mwangi wa fadhili.
Hakututenda sawasawa na hatia zetu,
Wala hakutulipakwa kadiri ya maovu yetu.(Kiitikio)

4. Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi,
Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.
Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake,
Ndivyo Bwana anavyowahurumia wamchao.(Kiitikio)